


HALMASHAURI YA WILAYA YA NYASA

(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W)
MKOA WA RUVUMA

Anwani ya Simu: "NYASA
COUNCIL"
Ofisini Simu Na: 025 - 2952003
Fax Na: 025 - 2952005
Nyumbani: 025 -
Email: ps.ded@nyasadc.go.tz



OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S. L. P. 90,
MBAMBA-BAY,
RUVUMA.

Unapojobu tafadhali taja:

Tarehe:16-08-2019

T A N G A Z O

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa anatangaza Zabuni ya kukodi magari kwa ajili ya kusambaza Mitihani ya kuhitimu Darasa la Saba Mwezi Septemba,2019. Maombi ya zabuni hii kutoka kwa Watu binafsi,Taasisi mbalimbali na wenge magari yenye sifa zifuatazo yanakaribishwa;-
 - a. Gari liwe ni aina ya "station wagon au hard top"
 - b. Gari liwe na nafasi ya kubeba watu 8 – 12.
 - c. Gari liwe na dereva mwenye leseni iliyo hai na halali.
 - d. Gari liwe na Bima.
 - e. Gari liwe katika hali nzuri ya kukabiliana na milima na mabonde.
2. Maombi kwa waliokidhi sifa zilizotajwa wafike kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)-Nyasa (Kata ya Kilosa) kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 jioni tarehe **16/08/2019(Ijumaa) – 21/08/2019(Jumatano)** kwa ajili ya kuchukua **fomu za maombi**.Fomu za maombi zinapatikana **bila malipo** kutoka ofisi ya Kitengo cha Manunuza na Ugavi.

Maombi hayo yaandikwe na kutumwa kwa;:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa

S.L.P 90. MBAMBA BAY

4. Kotesheni zote ziwe na nakala mbili (original 1 na copy 1) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa "Kotesheni Na. **LGA/145/2019-2020/NC/MV/ED/01 [Zabuni ya ukodishaji wa Magari kwa ajili ya Mitihani ya Darasa la Saba]** Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Kata ya Kilosa (Bomani) S.L.P 90 Mbamba bay.

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni Jumatano ya tarehe 21 – 08 - 2019 kabla ya Saa tisa na nusu (9.30 pm) jioni. Kotesheni zitafunguliwa hadharani kuanzia Saa tisa na nusu (9.30 pm) jioni mbele ya waombaji/wawakilishi watakaoamua kuhuduria katika ufunguaji wa Zabuni katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa [Nyasa bomani] zilizopo Kata ya Kilosa, S.L.P 90 Mbamba bay
6. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa Tathmini (Evaluation).
- Maelezo zaidi yanapatikana katika ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi pia katika fomu za maombi.

